


**Na: 25. Msimu wa Kilimo 2018/19 Tathmini ya Kipindi cha Mei 21-31, 2019 na Matazamio kwa Kipindi cha Juni 1-10 2019**

**Muhtasari**

- Mazao kwa maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka yameendelea vizuri.
- Hali ya ukavu inayotarajiwa itasaidia kukausha mazao ambayo tayari yamekomaa .
- Wakulima na wafugaji wanashauliwa kufuata ushauri unaotolewa na maafisa ugani ili wanufaike na utabiri huu.

**MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA  
KIPINDI CHA MEI 21-31, 2019**

**K**atika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) ilidhoofika wakati ile iliyopo kusini (St. Helena na Mascarene) iliendelea kuimarika. Hali hii ilisababisha ukanda wa mvua (ITCZ) kupanda kuelekea kaskazini mwa dunia na kuwepo katika nchi yetu hususan maeneo ya ziwa Viktoria. Joto la bahari la juu ya wastani katika eneo la kusinimagharibi mwa bahari ya Hindi liliendelea na kupelekea upepo wenye unyevunyevu kuvuma kutoka Kusini Mashariki hususani pwani ya kaskazini mwa Tanzania. Joto la bahari la chini kidogo ya wastani liliendelea katika eneo la Kusinimashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola). Hali hii ya mifumo ilipelekea kuimarika kwa mifumo ya mvua kwa baadhi ya maeneo ya nchi yetu hususani katika ukanda wa ziwa Viktoria.



Kielelezo: Kiasi cha mvua katika kipindi cha Mei 21- 31, 2019

**MWENENDO WA MVUA KATIKA KIPINDI CHA  
MEI 21-31, 2019**

**K**wa kipindi hiki mifumo imepelekea mvua za wastani katika maeneo ya ukanda wa ziwa viktoria na ,Pwani ya kaskazini ,na visiwa vya unguja na pemba na maeneo mengine ya nchi yameendelea kupata kiasi cha mvua chini ya wastani. Kiasi cha mvua cha 26 mm mpaka 100 mm kimepatikana katika baadhi ya maeneo ya ukanda wa Ziwa Viktoria na pwani ya kaskazini. Maeneo mengine ya nchi hususan pwani ya kusini, nyanda za juu kaskazin mashariki, Mikoa ya kati, Mikoa ya magharibi, nyanda za juu kusini magharibi na mikoa ya kusini yamepata kiasi cha mvua cha chini ya 26mm kama inavyojieleza kwenye ramani

**TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA  
KIPINDI CHA MEI 21-31, 2019**

**K**atika kipindi hiki cha dekad, baadhi ya maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka wakulima wengi walikuwa wanajihusisha na uvunaji wa mahindi isipokua kwa mikoa ya Njombe, Iringa na Mbeya ambako zao la mahindi liko katika hatua ya kukomaa. Zao la maharage limeripotiwa kuwa katika hali nzuri kwenye hatua ya kubeba na ngano iko kati mbalimbali za ukuaji na kubeba kwa mikoa ya Iringa, Njombe na Mbeya. Kwa maeneo mengi yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka hususan mkoa wa Kagera shughuli za uvunaji zimeanza. Kwa upande mwingine uvunaji wa mpunga uliendelea katika mikoani ya Tabora, Mwanza, Rukwa, Tanga na Manyara. Wakulima mkoani Kigoma, Mwanza, na Shinyanga wanaendelea na uvunaji wa pamba. Maji na malisho ya mifugo nchini kwa ujumla viliendelea kua katika hali nzuri isipokua kwa mkoa wa Dodoma ambako kumejitokeza upungufu kiasi.

### HALI YA MAJI ILIVYOKUWA KATIKA KIPINDI CHA MEI 21-31, 2019

**K**ina cha maji katika mabwawa na mitiririko ya maji kwenye mito kwa maeneo yaliyoendelea kupata mvua kiliendelea kuongezeka kutokana na mvua zilizoendelea kunyesha.

### MIFUMO YA HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA JUNI 1-10, 2019

**K**atika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia inatarajiwa kuendelea kupungua nguvu wakati ile iliyopo kusini inatarajiwa kuendelea kuimarika. Hali hii inatarajiwa kusababisha ukanda wa mvua kupanda kuelekea kaskazini mwa dunia na kuwepo katika nchi yetu hususan maeneo ya Ziwa Viktoria. Joto la bahari la juu ya wastani la kusini magharibi mwa Bahari ya Hindi linatarajiwa kuendelea, hali hii inatarajiwa kusababisha kufanyika kwa migandamizo midogo ya hewa pamoja upepo wenye unyevunyevu kuvuma kutoka kusini mashariki na kuelekea pwani ya kaskazini mwa Tanzania, hivyo kusababisha mvua kubwa hususani katika visiwa vya Unguja na Pemba. Joto la bahari la chini kidogo ya wastani linatarajiwa katika eneo la kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola). Hali hii ya mifumo inaweza kupelekea kuimarika kwa mifumo ya mvua kwa baadhi ya maeneo ya nchi yetu hususani katika ukanda wa Ziwa Viktoria na magharibi mwa nchi.

### HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA JUNI 1-10, 2019

**K**aeneo ya kanda ya ziwa Victoria yanatarajiwa kupata mvua zinazoambatana na ngurumo katika baadhi ya maeneo hususan siku tano za mwanzo wa dekad.

Maeneo ya nyanda za juu kaskazini mashariki yanatarajiwa kupata mvua katika maeneo machache hususan katika siku tano za mwanzo wa dekad.

Maeneo ya Pwani ya kaskazini yanatarajiwa kupata mvua katika maeneo machache, na kuongezeka kwa mvua siku mbili za mwisho wa dekad hususan katika visiwa vya Unguja na Pemba.

Maeneo ya magharibi mwa nchi yanatarajiwa kupata mvua zinazoambatana na ngurumo katika maeneo machache ya mkoa wa Kigoma na katika mikoa ya Tabora na Katavi kunatarajiwa kuwa na hali ya ukavu kwa ujumla.

Maeneo ya kanda ya kati, Nyanda za juu Kusinimagharibi, Pwani ya kusini na Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma na Maeneo ya kusini mwa Morogoro) yanatarajiwa kuwa makavu kwa ujumla.

### MATARAJIO NA USHAURI KWA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA JUNI 1-10, 2019

**M**ali ya mvua inayotarajiwa kwa maeneo mengi yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka (pwani ya kaskazini, Nyanda za juu kaskazini-mashariki, ukanda wa ziwa viktoriana) na mkoa wa Kigoma itaongeza hali ya unyevunyevu wa udongo. Ingawaje hali hii ya unyevunyevu haitaathiri hali ya mazao kutokana na msimu wa mvua kuelekea mwisho. Hali ya ukavu inayotarajiwa kwa maeneo ya kati (Dodoma na Singida), magharibi mwa nchi (Katavi na Tabora), nyanda za juu kusini magharibi, mikoa ya kusini na pwani ya kusini itafaa kwa mazao yaliyokatika hatua ya kukomaa na uvunaji. Mvua zinazoendelea kunyesha inchini hazitegemewi kudumu kwa kipindi kirefu kwa hyo wakulima na wafugaji wanashauriwa kufuata ushauri wa kitaalam kutoka kwa maafisa ugani katika maeneo yao ili kunufaika na mvua zilizotabiriwa.

### HALI YA MAJI INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA JUNI 1-10, 2019.

**K**ina cha maji katika mabwawa na mitiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kuwa vya wastani katika sehemu nyingi nchini. Hata hivyo, wananchi wanashauriwa kutumia maji hayo kwa uangalifu hususan maeneo ambayo huwa yanakabiliwa na upungufu wa maji.

Jarida limetayarishwa na:

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania  
Ghorofa ya 3-Ubungo Plaza – Barabara ya Morogoro, Dar es Salaam-Jamhuri ya Muungano wa Tanzania